# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.4 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JUNI 2021

# SERIKALI YATOA AJIRA ZA WALIMU 6,949



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu akitangaza ajira za walimu 6,949 wa shule za msingi na sekondari katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika Mei 09, 2021 jijini Dodoma. Pembeni yake ni Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# Utaratibu uzingatiwe upandishaji vyeo Walimu

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali kuwapandisha vyeo/madaraja watumishi wa Umma wenye sifa nchi nzima.

Watumishi wa Umma hususan Walimu walipokea agizo hilo kwa shangwe wakiona kuwa limekuja wakati muafaka ili kumaliza malalamiko yaliyokuwepo kuhusu kukaa kwenye daraja moja kwa muda mrefu.

Kazi inayoendelea sasa ni kwa Mamlaka zinazohusika na zoezi hilo kuwapandisha madaraja watumishi kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa namna ya kuwabaini watumishi wenye sifa za kupanda vyeo.

Kwa Upande wa Walimu, Kamati za TSC ngazi ya Wilaya ndizo zenye mamlaka ya kutekeleza jambo hilo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2016.

Hata hivyo, ni wajibu wa Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya pamoja na watendaji walio chini yake ambao ndio Sekretarieti ya Kamati za TSC za Wilaya kuhakikisha wanatoa ushauri unaotakiwa ili Kamati ziweze kutoa uamuzi wa haki na unaozingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Tuna imani kuwa Kamati za TSC zinaendesha zoezi la upandishaji madaraja walimu kwa haki na kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa. Hivyo, hatutarajii kusikia malamiko ya walimu walioachwa kwenye zoezi hilo huku wakiwa na sifa za kupanda madaraja.

Tafadhali tuandikie:

*Mhariri,*
*Sauti ya TSC,*
*Ofisi ya Rais,*
*Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC),*
*S.L.P. 353 – Dodoma*
*Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz*


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon


## KATUNI



# SERIKALI YATOA AJIRA ZA WALIMU 6,949



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu akitangaza ajira za walimu 6,949 wa shule za msingi na sekondari katika mkutano wake na waandishi wa habari (hawapo pichani) uliofanyika Mei 09, 2021 jijini Dodoma.*

**Na Adili Mhina.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu ametangaza nafasi za ajira za walimu 6,949 wa Shule za Msingi na Sekondari zinazolenga kujaza nafasi wazi za watumishi waliokoma utumishi wao kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kuacha kazi, kufukuzwa kwenye utumishi na kustaafu.

Waziri Ummy alitoa kauli hiyo Mei 9, 2021 wakati alipofanya mkutano na waandishi wa habari katika ofisi za TAMISEMI jijini Dodoma kwa lengo la kutoa taarifa ya ofisi yake kupata kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

"Tumepata kibali cha ajira za walimu 6,949 pamoja na watumishi 2,726 wa Kada ya Afya. Hivyo, nachukua fursa hii kuutangazia umma kuwa taratibu za kuanza mchakato wa kuomba ajira hizo umekamilika na kwamba waombaji wote wenye nia ya kuomba, sasa wanaweza kufanya hivyo", alisema.

Alifafanua kuwa waombaji wanatakiwa kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi ajira.tamisemi.go.tz kuanzia Mei 09 hadi 23 mwaka huu.

Hata hivyo, alieleza kuwa kwa upande wa watu wenye ulemavu hawatalazimika kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao badala yake watatuma maombi yao yakiwa katika nakala ngumu.

"Kwa ndugu zetu wenye ulemavu wanaweza kutuma maombi yao kwa nakala ngumu. Maombi hayo yaeleze aina ya ulemavu na yaambatane na picha kisha yatumwe kwa Katibu Mkuu TAMISEMI. Nakala ya Maombi hayo itumwe Ofisi ya Waziri Mkuu



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwa katika mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na waandishi wa habari uliofanyika Mei 09, 2021 jijini Dodoma.*

# SERIKALI YATOA AJIRA ZA WALIMU 6,949

ili Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu wenye Ulemavu aione.

Waziri Ummy alisema Ofisi yake imebainisha sifa mbalimbali za kitaaluma ambazo waombaji wanapaswa kuwa nazo kulingana na muundo wa kada ya ualimu wa shule za msingi na sekondari nchini.

Akianza kueleza sifa zinazotakiwa kwa walimu wa shule za msingi, Waziri Ummy alisema katika nafasi ya Mwalimu Daraja IIIA, mwombaji anatakiwa kuwa mhitimu wa Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Michezo, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Astashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum.

Aliongeza kuwa mwalimu Daraja la IIIB anatakiwa mhitimu mwenye Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali, Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi na Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum.

Vilevile, alisema kuwa katika nafasi ya Mwalimu Daraja la IIIC anatakiwa mhitimu mwenye Shahada ya Ualimu katika masomo ya "English Language, History na Geography".

Kwa Upande wa shule za sekondari, Ummy alifafanua kuwa nafasi ya Mwalimu Daraja la IIIB inahitaji mhitimu wa Stashahada ya Ualimu wa masomo ya "Physics, Mathematics, Biology na Chemistry".

Pia, katika nafasi ya Mwalimu Daraja la IIIC mwombaji anatakiwa kuwa na sifa mojawapo kati ya Shahada ya Ualimu, Shahada ya Elimu Maalum na Stashahada ya Uzamili katika Elimu (Post Graduate Diploma in Education) katika masomo ya "Physics, Chemistry, Biology na Mathematics".

Waziri ummy aliongeza kuwa kwa waombaji waliopata elimu Nje ya Nchi, wanatakiwa kuzingatia taratibu zilizowekwa za kupata uthibitisho wa elimu zao kwa mamlaka zinazohusika kabla ya kuomba ajira hizo.

"Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari Nje ya Nchi wanatakiwa kupata namba ya ulinganifu wa matokeo kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA). Waombaji waliosoma Vyuo Nje ya Nchi wanatakiwa kupata Ithibati ya masomo yao kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Ummy alisisitiza kuwa kila mwombaji ni lazima awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45, awe na namba ya kitambulisho cha Taifa, awe na vyeti kamili vya mafuzo ya fani aliyosomea na asiwe mwajiriwa wa Serikali au aliyewahi kuajiriwa na Serikali.

Mkutano huo wa Waziri na Waandishi wa Habari ulihudhuriwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama ambaye Ofisi yake ndiyo Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa katika utumishi wa Umma.



*Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, anayesimamia Elimu ya Awali na Msingi, ambaye pia ni Kamishna wa TSC, Susan Nussu, akiwa katika mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na waandishi wa habari uliofanyika Mei 09, 2021 jijini Dodoma.*

# TSC YAHAMASISHWA KUHAKIKISHA WALIMU HAWAONDOKI KAZINI



*Afisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Mwl. Martin Nkwabi, akifungua mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) zilizoko Kanda ya Ziwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza. Kulia ni Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba.*

**Na Veronica Simba – TSC**

Watendaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamehamasishwa kubuni mbinu zitakazowafanya walimu waache kukiuka maadili ya kazi yao, suala ambalo husababisha wengi kupata adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuzwa kazi.

Wito huo ulitolewa Aprili 28 mwaka huu na Afisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Mwl. Martin Nkwabi, wakati akifungua mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo.

"TSC hakipaswi kuwa chombo cha kusubiri mashauri. Lazima muwe na utaratibu wa kuhakikisha walimu hawafanyi makosa yanayosababisha kuondolewa kazini," alisisitiza.

Kuhusu suala la maadili, Mwl. Nkwabi aliishauri TSC kuzifikia shule zote kwa lengo la kuhakikisha walimu wanazingatia maadili ya kazi yao kwa kuwalea vema wanafunzi ili wawe raia wema.

Alisema kuwa ni wajibu wa walimu kusimamia maadili na makuzi ya wanafunzi hivyo TSC ikiwa ni Mamlaka yao ya Nidhamu, inapaswa kuhakikisha wajibu huo unatekelezwa



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Willy Komba, akitoa neno la kumkaribisha Afisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Mwl. Martin Nkwabi, ili afungue mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama, akitoa taarifa ya utangulizi kabla ya Afisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Mwl. Martin Nkwabi, kufungua mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*

# TSC YAHAMASISHWA KUHAKIKISHA WALIMU HAWAONDOKI KAZINI

kikamilifu.

Afisa Elimu huyo alikemea tabia ya baadhi ya walimu kuwachukulia wanafunzi kama wateja wao hivyo hawashughuliki na malezi yao wakiamini kuwa mteja hakemewi kwani ndiye anawawezesha kupata mshahara.

"Siku walimu wote wakiwaangalia wanafunzi kama watoto wao wa kuzaa, tunaweza kuondokana na tatizo hili."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba, akitoa neno la kumkaribisha Mgeni Rasmi, aliwaasa watendaji wa Tume hiyo kuhakikisha wanatenda haki kwa walimu kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo, ili nao waweze kuwalea wanafunzi vema.

"Walimu bora ndiyo watazaa elimu bora. Walimu bora lazima wahudumiwe vizuri. Bila kuwahudumia walimu vizuri watakuwa na manung'uniko na kero na hawatafanya kazi vizuri. Ndiyo maana Serikali ikatuamini sisi tuwahudumie," alisisitiza Prof.



*Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape, akiwasilisha mada kuhusu Kusudi la kuanzishwa kwa Tume hiyo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*

Komba.


Akitoa neno la utangulizi, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alitoa shukrani kwa Mungu na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumwamini na kumteua kushika wadhifa huo, hivyo aliahidi kuitumikia nafasi hiyo kwa uadilifu na weledi ili asimwangushe Rais.

Akizungumzia mafunzo husika, Mwl. Nkwama alieleza kuwa ni zoezi endelevu ambalo litaendelea katika Kanda zote saba zinazohudumiwa na TSC kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati husika waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

"Ni matarajio yetu kuwa baada



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Suzan Nussu akifafanua jambo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama, akiwasilisha mada kuhusu Muundo na Majukumu ya Tume hiyo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*

# TSC YAHAMASISHWA KUHAKIKISHA WALIMU HAWAONDOKI KAZINI



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Richard Odongo, akifafanua jambo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mectildis Kapinga, akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya Tume kuhusu masuala ya ajira na maendeleo ya walimu wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimaliwatu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Shani Kamala akizungumza jambo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zilizoko Kanda ya Ziwa, Aprili 28, 2021 jijini Mwanza.*

ya mafunzo haya, Wajumbe wa Kamati husika watakwenda kutatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu, ili kuwawezesha kutimiza majukumu yao ya kuwalea wanafunzi ipasavyo kimwili, kiakili, kijamii na kiroho."

Mafunzo hayo ya siku mbili yalishirikisha Wajumbe kutoka Wilaya zote za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, ambazo ni Mara, Geita, Simiyu, Kagera na Mwanza.



*Sehemu ya washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) zilizoko Kanda ya Ziwa, wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa katika mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Mwanza, Aprili 28, 2021.*

# WALIMU WAASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA NIDHAMU



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea katika mkutano wake uliowahusisha Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba (hawapo pichani) wakati wa ziara yake iliyofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

**Na Adili Mhina.**

Walimu wametakiwa kufanya kazi kwa bidii, weledi na kuzingatia miiko na maadili ya kazi hiyo ili kufikia malengo ya Serikali katika kuogeza ufaulu wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini.

Kauli hiyo imetolewa Mei 18, 2021 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama katika ziara yake wilayani Iramba ambapo alifanya mkutano uliowahusisha Walimu, Wakuu wa Shule, Mwakilishi wa CWT, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Iramba, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora, Mwenyekiti wa Kamati ya TSC Wilaya ya Iramba pamoja na Maafisa Elimu wa Msingi na Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya elimu juu ya masuala mbalimbali ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu ili kuongeza kasi ya utendaji kazi wa walimu.

Nkwama alieleza kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi katika sekta ya elimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora, hivyo walimu hawana budi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu ili kupata matokeo yanayoendana na thamani ya fedha inayowekezwa.

"Lengo letu Kitaifa kwa upande wa taaluma ni kuhakikisha asilimia 90 ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba wanafaulu. Kwa kuwa Iramba ni miongoni mwa Halmashauri zilizopo vijijini, lengo lenu ni kuhakikisha asilimia 85 ya wanafunzi wanafaulu ikiwa ni pamoja na kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (kkk)," alisema.

Kwa upande wa sekondari, Nkwama alieleza kuwa ipo changamoto ya upungufu wa walimu katika masomo ya sayansi na hisabati lakini walimu wa masomo ya sanaa wapo kwa kiwango kikubwa, hivyo endapo walimu hao watatekeleza



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Iramba, Francis Kasian akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake katika Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

# WALIMU WAASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA NIDHAMU

wajibu wao vizuri, hakuna mwanafunzi atakayepata chini ya daraja la tatu kwenye matokeo ya mitihani ya Taifa.

"walimu wa Kiswahili, English, History, Geography na Civics tupo, hivyo tunatarajia kiwango cha chini cha ufaulu kwa kila somo kwa mwanafunzi kiwe ni C. Mwanafunzi akiwa na C tano tayari ana *Division three* hapo tutakuwa tumeondokana na *Division four* na *zero*," alisema.


Pamoja na malengo hayo ya ufaulu, Nkwama alisisitiza kuwa wanafunzi wanatakiwa wafaulu kwa haki na sio kutumia mbinu za udanganyifu wa mitihani jambo ambalo sio kwamba tu ni kinyume na sheria na taratibu za kazi bali pia linabomoa Taifa.



*Mwenyekiti wa Kamati ya TSC Wilaya ya Iramba, Shiwariael Marunda akitoa neno la ukaribisho katika Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

Alieleza kuwa walimu ndio wenye jukumu kubwa la kufanya malengo hayo yafikiwe, hivyo suala la nidhamu na maadili ni la msingi kwa kuwa mwalimu asiye na maadili hawezi kutimiza wajibu wake kama alivyopangiwa na Serikali.

"Mwalimu anayezingatia maadili ya kazi yake ndiye anayeweza kufanya kazi kwa bidii na kujituma. Mwalimu asiye na maadili atakuwa mvivu, mzembe na asiyejali kazi yake. Hivyo maadili na nidhamu ni jambo la kwanza katika kufikia malengo yaliyokusudiwa,"



*Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Manasseh Stephen akitoa salamu fupi wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*



*Afisa Utumishi anayeshughulikia masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akitoa mada wakati wa mkutano.*

# WALIMU WAASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA NIDHAMU



*Mwalimu Grace Kinyau wa Shule ya Msingi Lulumba akichangia mada wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*



*Mwalimu Edward Said wa Shule ya Msingi Igumo akiuliza swali kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani) wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

alisisitiza.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake katika Mkutano huo, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilayani hapo, Francis Kasian alieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ina jumla ya walimu 1,139 wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha shule za serikali.

Alisema kuwa kuanzia mwaka 2016 ofisi yake imeshughulikia mashauri ya nidhamu 61 ambapo mashauri 41 yalikuwa ni ya makosa ya utoro, 16 mahusiano ya mapenzi na wanafunzi na mashauri 4 yalikuwa ya makosa mbalimbali ya ukiukaji wa maadili ya kazi ya ualimu.

"Katika kushughulikia mashauri hayo, walimu 33 walifukuzwa kazi na 28 walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo kupunguziwa mshahara, kushushwa cheo na kusimamishiwa nyongeza ya mshahara baada ya kukutwa na hatia," alifafanua.



*Baadhi ya Walimu wakiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

Kasian alihitimisha kwa kusema kuwa kumekuwa na ushirikiano wa karibu kati TSC na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo katika kuwafikia walimu na kuwaelimisha juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wao, jambo ambalo limefanya mashauri ya nidhamu kuendelea kupungua.

Kwa pande wake Mwenyekiti wa Kamati ya TSC Wilaya ya Iramba, Shiwariael Marunda alieleza kuwa Kamati yake imekuwa ikifanya jitihada za maksudi katika kuwaelimisha

# WALIMU WAASWA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA NIDHAMU

walimu ili wasijiingize katika makosa ya kiutumishi.

"Tukiwa kwenye vikao vya kamati yetu, hakuna kitu kinachotuumiza kama kupokea shauri la nidhamu ambalo ukiliangalia linakwenda kupoteza ajira ya mwalimu. Kwa kweli tumejikita sana katika kuwaelimisha walimu waelewe sheria na taratibu za utumishi wao," alisema.

Naye Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Manasseh Stephen alieleza kuwa kuna baadhi ya walimu ambao walipata barua za kupandishwa vyeo mwaka 2016 lakini barua hizo zikafutwa kutokana na zoezi la uhakiki wa watumishi hewa na kuomba Serikali iwasaidie walimu hao waweze kupanda vyeo katika zoezi linaloendelea sasa.

"Ndugu Katibu kwa kuwa walimu hawa walichelewa kupanda madaraja katika kipindi cha nyuma baada ya kufutiwa barua walizokuwa wamepewa awali, ninaomba



*Baadhi ya Walimu wakiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC na Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba uliofanyika wilayani hapo Mei 18, 2021.*

muishauri Serikali ili walimu hao waweze kupanda vyeo katika zoezi la sasa," alisema Stephen.

Katika mkutano huo mada mbili ziliwasilishwa ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape aliwahimiza walimu kuzingatia Nguzo za kazi ya ualimu ambazo zinamtaka mwalimu kutoa malezi na taaluma bora kwa wanafunzi, kuwajibika kwa mwajiri wake, kuwajibika kwa Taifa pamoja na kuwa na uzalendo.

Katika mada nyingine iliyowasilishwa na Afisa Utumishi anayeshughulikia masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa alieleza kuwa mwalimu anayekaribia kustaafu anatakiwa kuomba kibali cha kustaafu miezi sita kabla ya tarehe yake ya kustaafu ili kuondoa usumbufu kwa mfuko wa hifadhi ya jamii katika kushughulikia mafao yake.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa TSC Makao Makuu, TSC Iramba pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Pichani, upande wa kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape na kushoto ni Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Chacha Kehogo.*

# NAIBU KATIBU MKUU TAMISEMI ANENA JAMBO UPANDISHAJI MADARAJA WALIMU

**Na Veronica Simba – TSC**



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli akizungumza na washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu, yaliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni. Kushoto ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba na kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli ametoa maelekezo kuwa upandishaji madaraja kwa walimu uzingatie sifa zao katika kazi, hususan utendaji mahiri.

Alitoa maelekezo hayo hivi karibuni, wakati alipozungumza na washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu, yaliyofanyika jijini Mwanza.

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), yalilenga kuwawezesha washiriki kufahamu na kutekeleza majukumu yao ya Tume kwa haki.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa hotuba ya kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu – TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Gelard Mweli (wa pili-kushoto) ili azungumze na washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu, yaliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni. Wengine pichani kutoka kulia ni Kamishna wa TSC kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) Assela Luena, Kamishna wa TSC kutoka TAMISEMI Suzan Nussu na Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama.*

Akifafanua, Naibu Katibu Mkuu Mweli alisema kuwa, zipo sifa kadhaa zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa upandishaji madaraja ambazo alizitaja baadhi kuwa ni pamoja na muda ambao mtumishi amekuwa kazini na utendaji kazi wake.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa ni muhimu zaidi kuzingatia utendaji kazi wa Mwalimu kama sifa kuu ya upandishaji Daraja.

"Ukimpandisha Daraja asiyefanya kazi vizuri, ukamwacha mtendaji mzuri, unamvunja moyo anayefanya vizuri lakini pia inachangia kushusha hadhi ya taaluma ya ualimu," alisisitiza.

Mweli aliendelea kusisitiza

# NAIBU KATIBU MKUU TAMISEMI ANENA JAMBO UPANDISHAJI MADARAJA WALIMU



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati Naibu Katibu Mkuu – TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Gelard Mweli (wa tatu-kushoto) alipowatembelea na kuzungumza na washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu, yaliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni. Wengine pichani kutoka kushoto ni Afisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza Mwl. Martin Nkwabi, Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba, Makamishna wa TSC Suzan Nussu kutoka TAMISEMI na Assela Luena kutoka NACTE.*

kuwa, ni vema kabla Mwalimu hajadai kupandishwa Daraja, ajitathmini utendaji wake kama anafaa kupanda au la.

Alisema iko mifano hai kadhaa ambapo baadhi ya Walimu wenye muda mfupi kazini wamekuwa watendaji mahiri kushinda wenye muda mrefu kazini, hivyo akasisitiza kuwa uwepo wa muda mrefu kazini usitumike kama kigezo pekee cha kumpandisha Mwalimu Daraja isipokuwa sifa hiyo iende sambamba na utendaji kazi.

Katika hatua nyingine, Naibu Katibu Mkuu aliwataka watendaji wa TSC kushughulikia masuala ya walimu kwa haki, weledi na kwa wakati.

Alisema kuwa TSC ilianzishwa ili iwe Mkombozi kwa walimu na siyo kinyume chake hivyo akawataka watendaji katika ngazi zote kuwajibika ipasavyo ili walimu wajivunie uwepo wake.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi wa TSC, Katibu wake Mwl. Paulina Nkwama, alimhakikishia Naibu Katibu Mkuu kuwa, Tume itazingatia maelekezo yote aliyoyatoa ili kuendelea kutoa huduma nzuri kwa Walimu ambao ndiyo wadau wake wa kwanza.

Naye Mkurugenzi Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape, alimweleza Naibu Katibu Mkuu kuwa, TSC imejiwekea utaratibu wa ndani ambapo inahakikisha mashauri yote ya Walimu yanashughulikiwa ndani ya muda mfupi zaidi kulinganisha na ule uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mafunzo hayo yalihusisha Wilaya zote kutoka Mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu na Geita.



*Washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu, wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli (hayupo pichani) alipofika kuwatembelea na kuzungumza nao wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni.*

# NKWAMA: PANDISHENI WALIMU MADARAJA KWA KUZINGATIA MWONGOZO WA SERIKALI

**Na Adili Mhina**



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akisaini daftari la wageni katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ukerewe wakati wa ziara yake iliyofanyika Aprili 30, 2021.*

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama Aprili 30, 2021 alifanya ziara wilayani Ukerewe na kuwataka watumishi wa Tume hiyo kuhakikisha wanazingatia mwongozo uliotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kushughulikia upandishaji wa Madaraja ya walimu ili kuhakikisha haki inatendeka katika zoezi hilo.

Katika ziara hiyo ambayo aliambatana na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape pamoja na Mkurugenzi Msaidizi Maadili na Nidhamu, Robert Lwikolela, Nkwama alisema kuwa TSC imedhamiria kuondoa kero za walimu, hivyo ni lazima watumishi wa TSC wazingatie taratibu zilizowekwa na kujiepusha na masuala ya upendeleo wakati wa kutoa huduma kwa walimu.

Vilevile, Nkwama aliwataka watumishi wa TSC wilayani hapo kufanya ziara shuleni kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Christina Hape akisaini daftari la wageni katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ukerewe wakati wa ziara ya Katibu wa Tume iliyofanyika Aprili 30, 2021.*

# NKWAMA: PANDISHENI WALIMU MADARAJA KWA KUZINGATIA MWONGOZO WA SERIKALI

juu ya msuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo yao ili walimu waweze kuwa na uelewa mpana juu ya wajibu na haki zao katika utumishi wa Umma.

Aliongeza kuwa kuwafikia walimu mara kwa mara na kuwapa elimu kunasaidia walimu kujiepusha na makosa ya kinidhamu ambayo baadhi yao wanayafanya kwa kukosa uelewa wa kutosha juu ya sheria kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

Alisisitiza kuwa kwa kuwa TSC haina vyombo vya usafiri vya kutosha katika ofisi za wilaya, watumishi wa wilayani wanapaswa kuwa na ushirikiano wa karibu na ofisi za Halmashauri, kufanya kazi kama timu moja na kufanya ziara pamoja na watumishi wa sekta ya elimu badala ya kukaa na kulalamika kuwa wanashindwa kufanya kazi kwa kuwa hawana vyombo vya usafiri.



*Katibu wa TSC Paulina Nkwama (wa pili kutoka upande wa kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Christina Hape (wa kwanza kushoto), Mkurugenzi Msaidizi Maadili na Nidhamu, Robert Lwikolea (wa kwanza kulia) pamoja na mtumishi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Magreth David (wa pili kutoka kushoto) wakati wa ziara ya Katibu wa Tume iliyofanyika Aprili 30, 2021.*

# WATUMISHI TSC WAKUMBUSHWA MAJUKUMU YAO

**Na Veronica Simba – TSC**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamekumbushwa majukumu yao wanayopaswa kuyatekeleza katika utendaji kazi wao wa kila siku na kutakiwa kutoenenda kinyume nayo.

Majukumu hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape, wakati akiwasilisha mada kuhusu kusudi la kuanzishwa kwa Tume hiyo kwa wajumbe wa Kamati za Wilaya za Kanda ya Ziwa zinazoshughulikia ajira na maadili, kwenye mafunzo yaliyofanyika jijini Mwanza hivi karibuni.

Akielezea majukumu hayo, Mkurugenzi Hape alisema ni pamoja na kuwatumikia walimu kwa bidii, uaminifu na kwa kujituma katika masuala ambayo Serikali imeipatia TSC kwa mujibu wa sheria, ili kupunguza malalamiko ya walimu na kuwafanya watekeleze majukumu yao ya ualimu kwa furaha.

Vilevile, alisema kuwa jukumu jingine la TSC ni kuhakikisha Waajiri wanazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Serikali katika kulipa stahili, kushughulikia masuala mbalimbali ya walimu na kuiepushia Serikali madeni yasiyo ya lazima.

Akieleza zaidi, alisema kwamba TSC pia inawajibika kutenda haki katika kutoa uamuzi wa masuala ya kinidhamu na rufaa kwa walimu pamoja na kubuni namna bora zaidi ya kuwapa motisha walimu ili wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Aliongeza kuwa, jukumu jingine ni kuelimisha walimu kuhusu masuala ya Tume, maadili, wajibu na haki za walimu katika utumishi wao.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Hape aliwaambia washiriki wa mafunzo hayo kuwa TSC ina imani na wajumbe wote wa kamati za wilaya zinazoshughulikia ajira na nidhamu kwa walimu.

"Iwapo kamati hizo zitawajibika vizuri, Tume itapunguza mzigo wa rufaa na malalamiko yanayowasilishwa na walimu," alisisitiza.

Aidha, aliwataka wajumbe wa kamati hizo wawe huru kuhoji na kuomba ufafanuzi ili kuwa na uelewa mzuri kabla ya kutoa uamuzi wowote kwenye vikao vya kisheria.

Alisema mafunzo hayo yalilenga kuwapa ufahamu na kujiamini zaidi katika kushughulikia masuala ya walimu.



*Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape, akiwasilisha mada kuhusu Kusudi la kuanzishwa kwa Tume hiyo wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zinazoshughulikia ajira na maadili ya walimu zilizoko Kanda ya Ziwa, yaliyofanyika hivi karibuni jijini Mwanza.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (kushoto) na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape, wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zinazoshughulikia ajira na maadili ya walimu zilizoko Kanda ya Ziwa, yaliyofanyika hivi karibuni jijini Mwanza.*

# MWALIMU NKWAMA: MAJALADA YA WALIMU NCHINI YANAINGIZWA KWENYE MFUMO

**Na Mwandishi wetu**

Jumla ya majalada 367,022 yanatarajiwa kuingizwa kwenye mfumo wa kielekroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za waalimu unaoitwa E-Office ambapo mpaka sasa tayari majalada 20,000 yameingizwa kwenye mfumo huo yakiwemo ya upandishaji wa madaraja kwa walimu.

Kauli hiyo imetolewa Katibu waTume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama alipokutana na waandishi wa habari wakati alipofanya ziara wilayani Manyoni kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa zoezi la upandishaji vyeo walimu.

Nkwama amesema kuwa, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzisha mfumo huo ikiwa ni mbadala wa matumizi ya nakala ngumu.

Amesema kuwa,



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akisaini daftari la wageni katika Ofisi za TSC Wilaya ya Manyoni wakati wa ziara yake iliyolenga kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya TSC wilayani hapo.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwa katika mahojiano na waandishi wa habari juu ya utekelezaji wa zoezi la kuingiza majalada ya walimu kwenye mfumo wa kielektoniki. Mahojiano hayo yalifaniyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Wilaya ya Manyoni.*

Tume hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaendelea kujiimarisha katika suala la mifumo ili kurahisisha utendaji kazi wa tume hiyo.

Nkwama amesema kuwa, TSC inaendelea kujiimarisha katika mifumo ya utendaji kazi ambapo mfumo wa E-office unasaidia katika kuhakikisha mafaili yote yanaingizwa kwenye mfumo na kufanyiwa kazi.

Aidha, ameweka wazi kuwasiliana na Ofisi hiyo kupitia tovuti ambayo ni www.tsc.go.tz, barua

# MWALIMU NKWAMA: MAJALADA YA WALIMU NCHINI YANAINGIZWA KWENYE MFUMO

pepe *secretary@tsc.go.tz* na watasaidiwa kwa haraka zaidi.

Wakati huo huo, Mwalimu Paulina Nkwama ametoa rai kwa ofisi zote za Tume za Utumishi wa Walimu nchini kuhakikisha zoezi la upandishaji wa madaraja kwa walimu kuanzia ngazi ya Sekretarieti ihakikishe inafanya kazi kwa kufuata mwongozo, uliotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Pia amewataka kuhakikisha wanafanya zoezi hilo kwa weledi , ufanisi, haki na bila upendeleo lengo likiwa walimu wenye sifa wapande vyeo na ambao hawana sifa wajibidishe na kusubiri wakati mwingine.

Amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani kwa kuona umuhimu wa kutoa motisha kwa watumishi wa umma.

Aidha, amewataka walimu kuhakikisha wanafanya kazi kwa nguvu zao zote kwa kuwa ni wajibu wao kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha, weledi na ufanisi kwa kuhakikisha wanatoa elimu bora kwa wanafunzi.

Kaimu Katibu Msaidizi TSC Wilaya ya Manyoni, Hawa Rajabu amesema kuwa wanategemea kupandisha vyeo walimu 444 ambao ndio wenye sifa kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa.



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Manyoni pamoja na watumishi kutoka TSC Makao Makuu walioambatana naye katika ziara yake wilayani hapo. Pichani, watatu kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape na watatu kutoka kulia ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Manyoni, Hawa Rajab.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiongea na Watumishi wa TSC Wilaya ya Manyoni (hawapo pichani) wakati wa ziara yake wilayani hapo.*

# ZAIDI YA NUSU YA WALIMU UBUNGO KUPANDA MADARAJA



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape akiongea na watumishi wa TSC Wilaya ya Ubungo (hawapo pichani) wakati alipotembelea ofisi hiyo kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa zoezi upaandishaji wa madaraja kwa walimu.*

**Na Adili Mhina**

Zaidi ya nusu ya idadi ya walimu wote wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam watakuwa ni miongoni mwa watumishi wa Umma watakaopanda madaraja hivi karibuni baada ya Serikali kutoa vibali vya kupandisha madaraja Watumishi wa Umma nchi nzima.

Kwa mujibu wa taarifa za ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Ubungo, Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 3,253 wa shule za msingi na sekondari za Serikali. Katika idadi hiyo, walimu 2,184 ni wa msingi na 1,069 ni wa sekondani.

Katika zoezi la kupandisha madaraja walimu nchini, TSC Wilaya ya Ubungo imeeleza kuwa inatarajia kupandisha jumla ya walimu 1,733 ambapo walimu 1,152 ni wa shule za msingi na walimu 581 ni wa sekondari.

Idadi hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ubungo, Florah Kapange alipokuwa akitoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape kuhusu maendeleo ya zoezi la kupandisha madaraja walimu katika Wilaya yake.

"Baada ya kufanya uchambuzi tumepata walimu 1,733 wenye



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ubungo, Florah Kapange akiwa anapitia orodha ya walimu wenye sifa za kupandishwa madaraja.*

# ZAIDI YA NUSU YA WALIMU UBUNGO KUPANDA MADARAJA



*Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ubungo wakiwa katika zoezi la kuandaa orodha ya walimu wenye sifa za kupanda madaraja katika Wilaya hiyo.*

sifa za kupanda madaraja. Hivyo, ikama yetu tuliyonayo inatosha kabisa kuwapandisha walimu wote wenye sifa", alisema.

Alisema kuwa tangu kibali cha kuwapandisha madaraja walimu kitoke, watumishi wa TSC katika Wilaya hiyo wamekuwa wakifanya kazi muda wote ili kuhakikisha wanaendana na muda uliopangwa na Serikali katika kukamilisha zoezi hilo.

"Kama unavyotuona hapa tumekuwa na kazi kubwa ya kuchambua majalada ya walimu wote ili tubaini wale wenye sifa za kupanda. Na hadi sasa tupo katika hatua nzuri, tunakamilisha uchambuzi na tumeanza kuandaa orodha ya wale wanaotarajiwa kupanda ili tuiwasilishe kwenye Kamati ya Wilaya ambayo itakaa ndani ya siku mbili zijazo", alisema.

Alisisitiza kuwa Walimu wa Wilaya hiyo wasiwe na wasiwasi juu ya zoezi hilo kwani timu yake inafanya kazi kwa uangalifu mkubwa kuhakikisha kila mwalimu mwenye sifa ya kupanda daraja anapata haki yake.

"Nitumie fursa hii kuwaondoa hofu walimu wote wa Wilaya ya Ubungo kuhusu kupanda madaraja. Tuko makini sana, hatutamuacha hata mwalimu mmoja mwenye sifa ya kupanda," alisisitiza.

Naye Mkurugenzi Hape alieleza kuwa ameridhishwa na namna zoezi hilo linavyotekelezwa huku akiwasisitiza watumishi wa ofisi hiyo kuhakikisha wanazingatia miongozo na taratibu ili kila mwalimu apate anachostahili.

"Niwapongeze sana kwa namna mnavyoendelea na zoezi hili, natambua kuwa kazi hii inachosha maana idadi ya walimu ni kubwa na kazi inatakiwa ikamilike ndani ya muda mfupi. Lakini niwaombe sana msije mkafanya kazi kwa kulipua, TSC ipo kwa ajili ya walimu hivyo ni wajibu wetu kuwahudumia kwa ubora", alisema.

Hape alisema kuwa Rais

# ZAIDI YA NUSU YA WALIMU UBUNGO KUPANDA MADARAJA

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuondoa kero na malalamiko ya walimu yaliyodumu kwa muda mrefu kuhusu madaraja, ndiyo maana alitoa maelekezo kuhusu jambo hilo.

"Lazima tujue kwamba tusipofanya kazi kama inavyotakiwa hatutaeleweka. Yaani Rais amesikia kilio cha walimu na ametuelekeza tuwapandishe madaraja halafu sisi tugeuke kuwa kikwazo, hakuna mtu atakayetuvumilia. Kila mtu akitekeleza wajibu wake vizuri hatutasikia mwalimu anayelalamika kuhusu madaraja", Hape alisisitiza.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015, TSC ndiyo chombo kilichopewa mamlaka ya kusimamia ajira na maendeleo ya walimu ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kusajili walimu (wapya kazini), kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo/madaraja, kubadilisha cheo walimu waliojiendeleza kimasomo pamoja na kutoa vibali vya kustaafu kazi ya ualimu.



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (wa tatu kutoka kushoto mstari wa mbele, aliyevaa gauni) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa (TSC) Wilaya ya Ubungo wakati wa ziara yake wilayani hapo iliyolenga kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa zoezi la kupandisha madaraja walimu. Pembeni yake (mwenye miwani) ni Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya hiyo, Florah Kapange.*

# KAMATI ZA NIDHAMU KWA WALIMU SIMAMIENI HAKI HATA KAMA ITAWAGHARIMU – WAKILI ODONGO





*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo, akiwasilisha mada kuhusu Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu kwenye mafunzo ya wajumbe wa Kamati za Wilaya, Kanda ya Ziwa, Aprili 29, 2021 jijini Mwanza.*

**Na Veronica Simba – TSC**

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo, amewaasa wajumbe wa Kamati za Wilaya zinazosimamia Ajira na Maadili ya Walimu, kutenda haki wanaposhughulikia mashauri ya walimu, pasipo kujali mazingira magumu ambayo wakati mwingine yanaweza kuwaathiri wao pia.

Wakili Odongo alitoa wito huo Aprili 29, 2021 jijini Mwanza, wakati akiwasilisha mada inayohusu Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika mafunzo ya Wajumbe wa Kamati husika za Wilaya, Kanda ya Ziwa.

Akifafanua, alieleza kuwa sheria inawataka watendaji hao kusimamia haki hata pale inapotokea wanaotuhumiwa ni ndugu au rafiki zao.

"Shughulikieni mashauri ya walimu wanaotuhumiwa kwa kufuata haki. Kama haki inakutaka kupita katikati ya Mlima, pita hapohapo pasipo

# KAMATI ZA NIDHAMU KWA WALIMU SIMAMIENI HAKI HATA KAMA ITAWAGHARIMU – WAKILI ODONGO

kupindisha, hata kama itakugharimu wewe mwenyewe," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Wakili Odongo aliwasisitiza wajumbe hao kuhakikisha wanazingatia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na.25 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 katika kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya walimu.

Sambamba na hilo, alisema Kamati husika zinapaswa kuzingatia Taratibu Bora za Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2007 pamoja na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009.

Awali, wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba na Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, waliwasisitiza washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha kwamba wanaendelea kujenga taswira njema ya TSC kwa walimu kwa kutenda haki.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalilenga kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati husika ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kuwahudumia walimu kwa weledi.





*Wajumbe wa Kamati za Wilaya zinazoshughulikia Ajira na Nidhamu kwa Walimu, wakimsikiliza Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo, alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu kwenye mafunzo hayo yaliyoshirikisha mikoa ya Kanda ya Ziwa, Aprili 29, 2021 jijini Mwanza.*

# NSUNZA: ILALA TUMETENDA HAKI KATIKA KUPANDISHA MADARAJA WALIMU



*Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ilala, Janeth Nsunza akieleza jambo kwenye Kikao cha Kamati hiyo kilichokaa hivi karibuni kwa lengo la kuwapandisha vyeo walimu.*

**Na Adili Mhina.**

Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ilala, Janeth Nsunza amesema Kamati yake imetenda haki katika kupandisha vyeo/madaraja walimu ambapo jumla ya walimu 2367 wa Wilaya hiyo wamepandishwa.

Nsunza ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa kuhitimisha kikao cha Kamati hiyo kilichokaa kwa siku mbili kwa lengo la kupandisha madaraja walimu kama ilivyoelekezwa na Serikali.

"Kamati yangu ina wajumbe makini, tumefanya kazi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na kila mtu ametendewa kama sheria inavyotaka. Haikuwa kazi nyepesi hata kidogo lakini na tunamshukuru Mungu kila kitu kimekwenda vizuri, nina imani kuwa hakuna mwalimu wa Ilala atakayekuwa na malalamiko ya madaraja", alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na kauli aliyoitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan juu ya kupandisha vyeo watumishi wa umma, walimu wamekuwa na imani na matarajio kuwa kutakuwa na mabadiliko ya maslahi katika ajira zao, hivyo Kamati yake ina wajibu wa kufanya vizuri ili kukidhi matarajio hayo.

"Tangu tulivyoanza kazi tumeendelea kuperuzi na kuhakikisha kila daraja haachwi mtu, pale tulipogundua tuna jalada la mtu lakini kwenye orodha limerukwa au majina yao yanashida tumekwenda mbali zaidi kutafuta vielelezo ili kupata taarifa sahihi," alisema.

Nsunza amewatoa hofu walimu wa Wilaya hiyo na kusema kuwa waendelee kufanya kazi kwa moyo na wawe na imani kuwa Kamati yake imetekeleza kikamilifu agizo la Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na katika kipindi kifupi kijacho watapokea barua zao za kupanda madaraja.

Akifafanua idadi ya walimu waliopandishwa madaraja, Kaimu Katibu wa TSC wilayani hapo, Subira Mwakibete, alisema kuwa katika Jumla ya Walimu 2367 wa shule za msingi na sekondari waliopandishwa madaraja, walimu1362 ni wa shule za msingi na 1005 ni wa sekondari.

Alisema baada ya

# NSUNZA: ILALA TUMETENDA HAKI KATIKA KUPANDISHA MADARAJA WALIMU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilala, Subira Mwakibete akifafanua jambo wakati wa kikao cha Kamati ya TSC Wilaya ya Ilala kilichokaa hivi karibuni kwa lengo la kuwapandisha vyeo walimu, ambapo walimu 2367 wamepandishwa vyeo.*

Kamati kufanya uamuzi wake, kazi inayoendelea ni kuandaa barua za walimu pamoja na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za waliopandishwa vyeo kwa mamlaka zingine ili ziendelee na hatua zinazotakiwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape ambaye alikutana na Kamati hiyo wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya zoezi la kupandisha vyeo walimu, alisema kuwa ni muhimu pande zote zinazohusika katika madaraja ya walimu zifanye kazi kwa ushirikiano zaidi.

Hape alitaja baadhi ya taasisi zinazohusika moja kwa moja kwenye zoezi hilo kuwa ni TSC, Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango.

"Suala la promotion (upandishaji vyeo) kwa walimu si la TSC peke yake, sisi tunalianzisha tu na kutoa barua kwa mwalimu kuwa tumekupandisha. Lakini michakato mingine ya maslahi yao inaanzia kwa mwajiri, iende UTUMISHI hadi Wizara ya Fedha ambao ndio wenye fedha za kulipa mishahara" alisema Hape.

Aliongeza kuwa "uhusiano wetu unatakiwa uwe wa karibu zaidi, tufanye kazi kwa pamoja kwa kuelewana ili mwalimu aweze kuishi vizuri. Pale ambapo itatokea changamoto, ni vyema mawasiliano yafanyike haraka na wote tushirikiane kuitatua, lengo nikufanya mwalimu asiwe na manung'uniko", alisema.

Katika kusisitiza hilo, Hape amemtaka Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilayani hapo kuhakikisha ofisi yake inaongeza kasi katika kukamilisha taratibu zilizosalia ili kutoa fursa kwa mamlaka zingine kuendelea na hatua zao.

"Lazima ujipange vizuri kuhakikisha mambo yanakwenda harakaharaka. Unajua sasa hivi kila mtu anapambana watumishi wake waingizwe kwenye mfumo ili approvers (waidhinishaji) kule utumishi warekebishe mishahara yao kwa wakati. Lazima na wewe uhakikishe kazi yako inakamilika haraka ili wilaya yako isije ikabaki nyuma," alisisitiza.

Katika mwendelezo wa ziara hiyo, Mkurugenzi Hape alitembelea pia Wilaya za Temeke na Kigamboni ambapo aliridhishwa na utekelezaji wa zoezi hilo. Alisema kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ndio wenye idadi kubwa ya walimu, hivyo aliamua kufanya ziara hiyo ili kuona namna zoezi linavyokwenda.

# WALIMU WASIOTUMIA ZANA ZA KUFUNDISHIA WAONYWA

**Na Adili Mhina**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewataka walimu wanaofundisha wanafunzi bila kuzingatia taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kutumia zana za kufundishia kuacha tabia hiyo mara moja kwani kufanya hivyo ni kukiuka maadili na miiko ya kazi ya ualimu.

Onyo hilo limetolewa hivi karibuni na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alipofanya ziara ya kikazi katika Wilaya ya Singida ambapo pamoja na mambo mengine alifanya mkutano uliowahusisha walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Maafisa Elimu Msingi na Sekondari, Wathibiti Ubora wa Shule, Viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Kamati ya TSC na Watumishi wa TSC wote kutoka Wilaya ya Singida pamoja na Viongozi wa Elimu Mkoa wa Singida akiwemo Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia elimu, Mwl. Nelas Malungu.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea katika mkutano wake uliowahusisha wadau wa elimu (Walimu, Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu Msingi na Sekondari, Kamati na watumishi wa TSC pamoja na viongozi wa CWT) kutoka Wilaya ya Singida. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida, hivi karibuni.*



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape akiwasilisha mada wakati wa mkutano wa Katibu wa TSC na Wadau wa Sekta ya Elimu wa Wilaya ya Singida.*

Mkutano huo uliokuwa na mada mbalimbali ulilenga kuwajengea uwezo walimu juu ya kanuni na taratibu za utumishi wa walimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 pamoja na kanuni zake za mwaka 2016 ambazo ndizo zinazoongoza kada hiyo katika masuala ya ajira, maadili na maendeleo walimu.

Nkwama alisema kuwa kwa sasa kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya walimu hususan wanaofundisha shule za sekondari kuingia darasani kufundisha bila kutumia zana za kufundishia kama taratibu zinavyoelekeza jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kazi hiyo.

“Tulipita kwenye

# WALIMU WASIOTUMIA ZANA ZA KUFUNDISHIA WAONYWA



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Singida, David Brown akitoa taarifa ya utendaji kazi wa ofisi yake kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani) wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na wadau wa sekta ya elimu wa Wilaya ya Singida (hawapo pichani) uliofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida, hivi karibuni.*

shule zaidi ya 50 za msingi na sekondari kuangalia jinsi walimu wanavyotekeleza majukumu yao. Kwa upande wa walimu wa shule za msingi hatukuona changamoto sana kwenye matumizi ya zana hususan kwa madarasa ya awali, la kwanza na la pili Lakini kwa walimu wa shule za sekondari tuligundua hawatumii zana za kufundishia kama utaratibu unavyoelekeza," alisema.

Nkwama alifafanua kuwa utaratibu wa mwalimu kufundisha kwa kutumia zana zinazohitajika uliwekwa ili kumsaidia mwanafunzi kuelewa na kuwa na kumbukumbu nzuri ya kile anachofundishwa, hivyo ni lazima kila mwalimu azingatie utaratibu huo uliowekwa kumsaidia mwanafunzi.

Sambamba na hilo Nkwama alieleza kuwa pamoja na serikali kujitahidi kusambaza vitabu shuleni, walimu wengi hawafundishi kwa kutumia vitabu badala yake wanatumia uzoefu tu jambo ambalo ni miongoni mwa sababu zinazochangia wanafunzi kufanya vibaya katika masomo yao.

"Serikali imefanya kazi nzuri ya kuleta vitabu shuleni hivyo walimu wanapaswa kufundisha huku wakifanya rejea kwenye vitabu, pia ni muhimu kuwajengea wanafunzi tabia ya kusoma vitabu mbalimbali vya kiada za ziada ili kuongeza uelewa wa kile wanachofundishwa," alisema.

Alionya kuwa kila mwalimu azingatie taratibu za kazi ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi yote yanayotakiwa kabla ya kuingia darasani, kutumia zana zinazohitajika wakati wa kufundisha kulingana na somo na mada husika wakati kufundisha.

"Kuna walimu tumesahau wajibu wetu, ndiyo maana



*Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia elimu katika Mkoa wa Singida, Nelas Mulungu akitoa neno la shukrani kwa Katibu wa TSC wakati wa mkutano wa Katibu huyo na wadau wa sekta ya elimu wa Wilaya ya Singida uliofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida, hivi karibuni.*

# WALIMU WASIOTUMIA ZANA ZA KUFUNDISHIA WAONYWA

tumekutana hapa ili tukumbushane. Kama wote tukifundisha kwa kuzingatia taratibu, nina imani kuwa wanafunzi watafanya vizuri kitaaluma na kimaadili, na tutafikia malengo ya serikali", alisema.

Katibu huyo aliweka bayana kuwa TSC ina majukumu mengi ya kutekeleza ili kuboresha ustawi wa walimu na haipo kwa ajili ya kusubiri walimu wafanye makosa ili iwafukuze kazi kama baadhi ya wadau walivyokuwa wanaitazama Tume siku za nyuma.

"Hatupendi hata kidogo kuwafukuza kazi walimu, tumejikita sana katika kuwaelimisha walimu wetu ili wawe na mwenendo mzuri na watekeleze majukumu yao ipasavyo. Tunajua wengi wanaelewa na wanajirekebisha, wale ambao hawataki kubadilika hapo hatuna namna, inabidi sheria ichukue mkondo wake," alisema.



*Mwalimu Ruth Kiranga wa Shule ya Msingi Unyianga iliyopo katika Wilaya ya Singida, akiuliza swali kwa Katibu wa Tume (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa Katibu huyo na wadau wa sekta ya elimu wa Wilaya ya Singida.*



*Afisa anayeshughulikia masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa akiwasilisha mada wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na wadau wa Elimu wa Wilaya ya Singida uliofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida, hivi karibuni.*

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya ya Singida, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilayani hapo, David Brown alisema kuwa Wilaya hiyo inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambazo zina jumla ya Walimu 2,392.

Aliongeza kuwa katika zoezi linaloendelea la kupandisha vyeo watumishi wa Umma, Wilaya yake imepandisha vyeo walimu 1,351 idadi ambayo ni sawa na asilimia 56.5 ya walimu wote wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha shule katika Wilaya hiyo.

Kwa upande wa maadili, Brown alisema kuwa kumekuwa na mabadiliko chanya kwa walimu kutokana na ofisi yake kufanya kazi kwa ushirikiano na Ofisi ya Elimu kuanzia ngazi ya Mkoa, Wathibiti Ubora wa Shule, Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili pamoja na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) katika kuwaelimisha walimu kuzingatia miiko na maadili ya kazi

# WALIMU WASIOTUMIA ZANA ZA KUFUNDISHIA WAONYWA



*Mwalimu Gadiel Maree wa Shule ya Msingi Unyakumi iliyopo katika Wilaya ya Singida, akitoa maoni wakati wa mkutano wa Katibu wa TSC na wadau wa sekta ya elimu wa Wilaya ya Singida.*

hiyo.

"Mwaka 2018 kulikuwa na mashauri ya nidhamu 18, mwaka 2019 mashauri 12 na mwaka 2020 mashauri 13 na hadi mwezi mei mwaka huu 2021 tumefungua mashauri matatu tu, hii ni kwa sababu tumewafikia walimu wengi na kuwapa elimu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu Kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape alieleza kuwa walimu wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili hata ujazaji wa fomu za Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) uwe na uhalisia.

"Unachukua OPRAS ya mwalimu kila sehemu ukiangalia amejaziwa vizuri sana lakini ukija kukutana na matokeo ya wanafunzi anaowafundisha unakuta wana sifuri. Tunataka OPRAS iweze kutusaidia kujua kiuhalisia kama mwalimu ni mchapakazi kutokana na ubora wa wanafunzi wake," alisema.

Kwa upande wake Afisa anayeshughulikia Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa aliwakumbusha walimu hao kuwa na utaratibu wa kufuatilia taarifa za michango yao kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ili kuhakikisha usahihi wa michango yao na kama ikibainika kuna dosari wawasilishe taarifa kwa mwajiri ili ifanyiwe kazi mapema.

Naye Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Elimu mkoani hapo, Nelas Malungu alimshukuru Katibu wa TSC kwa kufika Wilayani hapo na kukutana na walimu na kusema kuwa elimu waliyoipata itasaidia kila mtu kuboresha utendaji wa kazi katika eneo lake.



*Baadhi ya Walimu wa Wilaya ya Singida wakiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC (hayupo pichani) na wadau wa sekta ya elimu wa Wilaya ya Singida. Mkutano huo umefanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida, hivi karibuni.*

# TSC YAELEZA MAMBO YANAYOWEZA KUMSABABISHIA MWALIMU KUHITIMISHIWA UTUMISHI WAKE

**Na Veronica Simba – TSC**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), imebainisha mambo kadhaa yanayoweza kumsababishia Mwalimu, hususan aliyeko katika Utumishi wa Umma, kuhitimishiwa kazi yake ya ualimu.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Mectildis Kapinga wakati akiwasilisha Mada kuhusu majukumu ya Tume katika masuala ya ajira na maendeleo ya walimu, wakati wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za Wilaya zinazoshughulikia ajira na maadili ya walimu, yaliyofanyika hivi karibuni jijini Mwanza.

Kapinga alieleza kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 9(1) (a) – (g) ya Kanuni za Utumishi wa Walimu za mwaka 2016, mambo yanayoweza kumsababishia Mwalimu ahitimishe kazi yake ya Ualimu ni pamoja na kustaafu kwa kutimiza umri kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa, sababu nyingine ni kustaafu kwa ugonjwa, kuachishwa kazi kwa masuala ya kinidhamu, kufariki, kuacha kazi kwa hiari, kustaafishwa kwa manufaa ya umma, kufutwa kwa Ofisi na kugombea nafasi za uongozi hususan wa siasa.

Akielezea kuhusu utaratibu unaotumika wakati Mwalimu anapohitimisha utumishi kwa kustaafu kwa lazima au hiari, Mkurugenzi Kapinga alisema ni pamoja na Ofisi za TSC, Ngazi ya Wilaya kuandaa maoteo ya kustaafu kazi walimu kwa kila mwaka wa fedha na kuwasilisha nakala Makao Makuu ya Tume pamoja na kwa Mwajiri.



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mectildis Kapinga, akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya Tume katika masuala ya ajira na maendeleo ya walimu wakati wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC, zinazoshughulikia masuala ya ajira na maadili kwa walimu, zilizoko Kanda ya Ziwa, hivi karibuni jijini Mwanza.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Ilemela, James Fundikira akiongoza zoezi la utambulisho kwa washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zinazoshughulikia ajira na maadili kwa walimu, zilizoko Kanda ya Ziwa. Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni jijini Mwanza.*

# TSC YAELEZA MAMBO YANAYOWEZA KUMSABABISHIA MWALIMU KUHITIMISHIWA UTUMISHI WAKE



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Rorya, Nuhu Mlekwa akiwasilisha Majumuisho wakati wa kuhitimisha mafunzo kwa Kamati za Wilaya za TSC zinazoshughulikia masuala ya ajira na maadili kwa walimu, zilizoko Kanda ya Ziwa. Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni jijini Mwanza.*

Mwalimu husika.

Katika hatua nyingine, Kapinga alieleza kuwa kustaafu kwa lazima au kwa hiari kunategemea tarehe ya kuzaliwa kwa mwalimu, ambapo anaruhusiwa kustaafu kwa hiari afikishapo umri wa miaka 55 na atalazimika kustaafu kwa lazima afikishapo miaka 60.

Aliongeza kuwa, endapo itatokea kwenye kumbukumbu za kuzaliwa, Mwalimu akawa alijaza mwaka bila tarehe, basi tarehe yake itakayotumika itakuwa Julai Mosi ya mwaka atakaostaafu.

"Aidha, ikitokea kuwa alijaza mwezi na mwaka bila tarehe, basi tarehe yake ya kuzaliwa itahesabika kuwa tarehe 15 au 16 ya mwezi huo," alifafanua Kapinga.

Alihitimisha kwa kueleza kuwa, endapo kutakuwa na mgongano wa tarehe ya kuzaliwa kwenye kumbukumbu za kiutumishi za mwalimu husika, tarehe itakayotambuliwa kuwa ni tarehe yake sahihi ya kuzaliwa ni ile inayompa umri mkubwa.

Vilevile, alieleza kuwa utaratibu mwingine unaotakiwa kufanyika ni kwa Mwalimu anayetarajia kustaafu kwa hiari au lazima, kutoa taarifa miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu kwake, ikiwa ni kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.

Aliongeza kuwa, Katibu wa Tume ngazi ya Wilaya, anatakiwa kuandika kibali cha kustaafu kazi na kibali hicho kipitishwe na Mwajiri kabla ya kukabidhiwa kwa



*Sehemu ya washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), zinazoshughulikia masuala ya ajira na maadili kwa walimu, zilizoko Kanda ya Ziwa, wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa katika mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Mwanza, hivi karibuni.*

# WALIMU 1,333 KINONDONI KUPANDA VYEO



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kinondoni, Theobald Kilindo akiwasilisha taarifa ya hatua ya utekelezaji wa zoezi la kuwapandisha vyeo walimu kwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Mkurugenzi huyo aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

**Na Adili Mhina.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kinondoni ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha zoezi la kupandisha vyeo/madaraja walimu 1,333 wa shule za msingi na sekondari wa Manispaa ya Kinondoni ambao wana sifa za kupanda vyeo kwa mujibu wa miongozo na taratibu za Serikali.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wa Wilaya hiyo, Theobald Kilindo wakati akitoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape juu ya hatua iliyofikiwa katika zoezi la kuwapandisha vyeo walimu wa Manispaa hiyo.

Kilindo alieleza kuwa ofisi yake imepitia hatua mbalimbali katika kufanya zoezi hilo, ambapo kila hatua ilifanyika kwa uangalifu mkubwa na pale zilipobainika changamoto ofisi yake iliwasiliana na mamlaka zingine kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi.

Alieleza kuwa zoezi hilo lilianza kwa mwajiri kuwasilisha orodha ya walimu waliopendekezwa kupandishwa vyeo ili ofisi yake iendelee na hatua zaidi kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

"Tulileletewa barua na Mkurugenzi iliyotutaka tuanze zoezi la kupandisha vyeo walimu. Tulipitia taarifa za walimu ili tuweze kubaini wenye sifa za kupanda vyeo. Tulianza zoezi la uchambuzi Mei 3 na kulihitimisha Mei 11," alisema.

Alieleza kuwa katika hatua ya uchambuzi walibaini dosari ndogondogo katika ujazaji wa fomu za Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) jambo ambalo liliwalazimu kuwasiliana na mwajiri pamoja na wakuu wa shule ili kuondoa kasoro hizo.

"Sio kwamba kuna madadiliko yoyote tuliyofanya kwenye OPRAS ila tuligundua kwamba wakati wa kujaza, wengi hawakuwa na uelewa wa kutosha wa nini kinatakiwa kijazwe wapi na kwa namna gani. Tuliona baadhi walikuwa wamekosea pale kwenye kutafuta wastani walikuwa wanaweka namba ambazo hazikuwa sahihi," Silindo alifafanua.

Aliendelea kufafanua kuwa, "baada ya taratibu zote kukamilika, Kamati ya TSC Wilaya ambayo ndiyo yenye wajibu kisheria wa kupandisha vyeo walimu, ilifanya kikao chake Mei 12, 2021 na kuwapandisha vyeo walimu 1,333 ambao ndio waliokuwa na sifa".

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape alieleza kuwa Serikali ilifanya jambo la busara kwa kuamua kuchukua Ikama za miaka mitatu na kuzifanyia kazi kwa pamoja kwa kuwa hatua hiyo inaondoa kabisa malalamiko ya madaraja kwa walimu.

Pamoja na kupongeza hatua hiyo, Hape alitoa wito kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kujitahidi kuwabadilishia mishara walimu mapema iwezekanavyo ili wakiingia

# WALIMU 1,333 KINONDONI KUPANDA VYEO



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape akisikiliza taarifa kutoka kwa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kinondoni, Theobald Kilindo (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Mkurugenzi huyo iliyolenga kufanya ufuatiliaji wa zoezi la uoandishaji vyeo walimu wa Manispaa ya Kinondoni.*

kwenye vyeo vipya mishahara yao nayo iwe imebadilika.

"Unajua ukimwambia mwalimu umepanda cheo anataka aone mshahara umebadilika, kumpatia karatasi (barua) ya kupanda cheo peke yake bila yeye kuona maslahi yake yameboreshwa haitakuwa na faida sana kwake. Hivyo, napenda niwaombe wenzetu wa UTUMISHI kuhakikisha wanafanya kila linalowezekana ili mishahara ya walimu iendane na vyeo vyao kwa wakati", alisema.

Manispaa ya Kinondoni ina Jumla ya walimu 2,922 wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha shule za Serikali, ambapo katika idadi hiyo, walimu 1939 ni wa shule za msingi na walimu 983 ni wa sekondari.



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Wilaya ya Kinondoni wakiwa wanamsikiliza Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani) wakati Mkurugenzi huyo alipotembelea ofisi ya TSC Wilaya ya Kinondoni kwa lengo la kukagua zoezi la upandishaji vyeo walimu.*

# PROF. KOMBA ATAKA TSC IONE FAHARI KUHUDUMIA WALIMU WENYE MAADILI

**Na Veronica Simba – TSC**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Profesa Willy Komba, ametoa hamasa kwa watendaji wote wa Tume hiyo kusimamia vema suala la maadili kwa walimu ili wajisikie fahari kuwahudumia.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akifunga mafunzo ya wajumbe wa kamati za wilaya katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia ajira na maadili kwa walimu, chini ya usimamizi wa TSC.

Akifafanua, Prof. Komba aliwataka washiriki wa mafunzo husika, wanaporejea katika vituo vyao vya kazi, kwenda kuwajibika kwa kuwakumbusha walimu maadili na



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akitoa hotuba ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, ambaye ni Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Willy Komba kufunga mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu, hivi karibuni jijini Mwanza.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba, akifunga mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu, hivi karibuni jijini Mwanza.*

miiko ya kazi yao.

Alisema kuwa, endapo Kamati hizo za Nidhamu zitafanikiwa kuwafikia walimu wote, TSC itafanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya walimu wanaolalamikiwa kukiuka maadili ya kazi yao.

"Sisi sote tuone fahari ya kuwahudumia walimu wenye maadili ambayo watayaambukiza kwa watoto wanaowafundisha na jamii kwa ujumla," alisema.

Aidha, Mwenyekiti huyo wa TSC aliwasisitiza washiriki wa mafunzo kujenga utaratibu wa kujisomea sheria, kanuni, taratibu, miongozo na nyaraka

# PROF. KOMBA ATAKA TSC IONE FAHARI KUHUDUMIA WALIMU WENYE MAADILI



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu, wakimsikiliza Mgeni Rasmi ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (hayupo pichani), wakati akifunga mafunzo hayo, hivi karibuni jijini Mwanza.*

za serikali kuhusu masuala mbalimbali wanayoyashughulikia ili kujiongezea ufahamu.

Vilevile, aliwataka wasisite kuomba ufafanuzi kutoka kwenye Ofisi au Mamlaka nyingine hususan katika masuala yenye changamoto ili kuepuka kukosea katika utendaji wao.

Awali, akitoa hotuba ya kumkaribisha Mgeni Rasmi kufunga mafunzo hayo, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alieleza kuwa lengo lilikuwa ni kuwawezesha washiriki kufahamu na kutekeleza majukumu yao ya Tume kwa haki.



*Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Suzan Nussu kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI (kushoto) na Luwena kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa katika mafunzo kwa Kamati za Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinazoshughulikia masuala ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu, jijini Mwanza, hivi karibuni.*

Mwl. Nkwama alizitaja mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo kuwa ni pamoja na Kusudi la kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, Muundo na Majukumu ya Tume pamoja na Majukumu ya Tume kuhusu masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu.

Aliongeza kuwa, mada nyingine zilizowasilishwa ni kuhusu Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu pamoja na Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akipokea kitabu cha Mkataba wa Huduma kwa Mteja cha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka kwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Omary Juma Kipanga wakati wa uzinduzi wa kitabu hicho uliofanyika Mei 6, 2021 jijini Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kulia) akimsikiliza Katibu mstaafu wa TSC, Winifrida Rutaindurwa wakati Katibu mstaafu huyo alipotembelea ofisi za TSC Mei 7, 2021.*



*Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigamboni wakimsikiliza Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape alipotembelea wilayani hapo kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa zoezi la upandishaji madaraja kwa walimu.*



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Wilaya ya Temeke wakiwa katika hatua za mwisho za utekelezaji wa zoezi la kuwapandisha madaraja walimu wa Wilaya hiyo.*

*Baadhi ya Watumishi wa TSC Wilaya ya Temeke wakiwa katika hatua za mwisho za utekelezaji wa zoezi la kuwapandisha madaraja walimu wa Wilaya hiyo.*





**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***